



JobSeeker Payment

JobSeeker Payment (Malipo ya Mtafuataji Kazi) hutoa msaada wa kifedha ikiwa una umri kati wa miaka 22 na wa kustahili Pensheni ya Wazee. Unaweza kuipata wakati huna kazi na unatafuta kazi.

Inapatikana pia wakati wewe ni mgonjwa au umejeruhiwa na huwezi kufanya kazi au kusoma masomo yako ya kawaida.

Ustahili kupata JobSeeker Payment

Unaweza kustahili JobSeeker Payment ikiwa unakidhi yote yafuatayo:

- una umri kati wa 22 na wa kustahili Pensheni ya Wazee
- unakidhi sheria za mkaazi
- unakidhi vipimo vya mapato na mali.

Utahitaji pia kukidhi mmojawapo ya hali zifuatazo:

- Huna kazi na unatafuta kazi, au huna kazi ya wakati wote. Hii inaweza kujumuisha ikiwa unafanya kazi ya muda au ya kibarua.
- Huwezi kufanya kazi au kusoma kwa muda mfupi kwa sababu ya jeraha au ugonjwa. Unaweza kutakiwa kutoa cheti cha matibabu.

Viwango vya malipo kwa JobSeeker Payment

Kiasi unachoweza kupata kinaweza kutofautiana, na kinategemea hali yako ya kibinafsi. Hii ni pamoja na:

- kama una mpenzi
- kama una watoto
- kiasi gani cha mapato wewe na mpenzi wako mmepata katika siku 14 zilizopita.

Ikiwa unapata mapato zaidi ya kiasi fulani, yanaweza kuathiri kiasi unachoweza kupata.

Jinsi ya kudai JobSeeker Payment

Unaweza kudai JobSeeker Payment mtandaoni kwa kutumia akaunti yako ya Centrelink mtandaoni kupitia myGov.

Ikiwa huna akaunti ya myGov au akaunti ya Centrelink mtandaoni, utahitaji kuzianzisha.

Unaweza kuanza dai lako kwa JobSeeker Payment hadi wiki 13 kabla hali yako inabadilika. Hii ingeweza kutokea ikiwa yoyote:

- utafanya kazi masaa machache zaidi na unakidhi kipimo cha mapato
- unajua utapoteza kazi yako.

Unaweza kuondoa dai lako wakati wowote ikiwa hali yako ya kipesa inabadilika.

Wakati utakapopata malipo yako ya kwanza

Utapata malipo yako ya kwanza karibu wiki 2 baada tumekubali malipo yako isipokuwa kipindi cha kusubiri kinatumika. Tutakuambia ikiwa una kipindi cha kusubiri na muda gani ambao utahitaji kusubiri.

Utahitaji pia kutoa taarifa ya mapato yako na ya mpenzi wako. Utahitaji kutoa taarifa ya mapato kila wiki 2.

Mabadiliko ya hali

Utatakiwa kutuambia kama hali yako inabadilika kwani inaweza kuathiri malipo yako. Hii inaweza kuwa pamoja na:

- habari yako ya kibinafsi na ya mawasiliano
- hali yako ya uhusiano
- hali yako ya kazi.

Kwa habari zaidi

- piga simu kwa **131 202** kuongea na mtu katika lugha yako
- nenda kwa **servicesaustralia.gov.au/jobseekerpayment** kupata habari zaidi katika Kiingereza
- nenda kwa **servicesaustralia.gov.au/yourlanguage** ambapo unaweza kusoma, kusikiliza au kutazama habari katika lugha yako
- tembelea kituo cha huduma.

Kumbuka: simu kutoka simu yako ya nyumbani kwenda nambari za '13' kutoka popote nchini Australia zinatozwa kwa kiwango kamili. Kiwango hicho kinaweza kutofautiana kutoka bei ya simu ya mtaa na kinaweza pia kutofatiana na watoaji huduma ya simu. Simu kwa nambari za '1800' kutoka simu yako ya nyumbani hazina malipo. Simu kutoka simu za umma na za mkononi zinaweza kupimwa kwa muda wao na kutozwa kwa kiwango cha juu zaidi.

Kanusho

Habari iliyomo katika chapisho hili linakusudiwa tu kuwa mwongozo kwa malipo na huduma. Ni wajibu wako kuamua ukitaka kuomba kwa malipo na kufanya ombi kuhusiana na hali yako maalum.

JobSeeker Payment

JobSeeker Payment provides financial help if you are between 22 and Age Pension age. You can get it while you are unemployed and looking for work.

It is also available when you are sick or injured and cannot do your usual work or study.

Eligibility for JobSeeker Payment

You may be eligible for JobSeeker Payment if you meet all of the following:

- you are between 22 and Age Pension age
- you meet the residence rules
- you meet the income and assets tests.

You will also need to meet one of the following situations:

- You are unemployed and looking for work, or not in full time work. This can include if you are doing part time or casual work.
- You are unable to work or study for a short time because of an injury or illness. You may need to provide a medical certificate.

Payment rates for JobSeeker Payment

The amount you can get may vary, and depends on your personal situation. This includes:

- if you have a partner
- if you have children
- how much income you and your partner earned in the past 14 days.

If you earn income over a certain amount, it may affect how much you can get.

How to claim JobSeeker Payment

You can claim JobSeeker Payment online using your Centrelink online account through myGov.

If you do not have a myGov account or Centrelink online account, you need to set them up.

You can start your claim for JobSeeker Payment up to 13 weeks before your circumstances change. This could be if either:

- you will be working less hours and meet the income test
- you know you will lose your job.

You can withdraw your claim at any time if your financial situation changes.

When you get your first payment

You will get your first payment around 2 weeks after we grant your payment unless a waiting period applies. We will tell you if you have a waiting period and how long you will need to wait.

You will also need to report your and your partner's income. You will need to report income every 2 weeks.

Change of circumstances

You need to tell us if your circumstances change as it could affect your payment. This may include:

- your personal and contact details
- your relationship status
- your work status.

For more information

- call **131 202** to speak to someone in your language
- go to **servicesaustralia.gov.au/jobseekerpayment** for more information in English
- go to **servicesaustralia.gov.au/yourlanguage** where you can read, listen to or watch information in your language
- visit a service centre.

Note: calls from your home phone to '13' numbers from anywhere in Australia are charged at a fixed rate. That rate may vary from the price of a local call and may also vary between telephone service providers. Calls to '1800' numbers from your home phone are free. Calls from public and mobile phones may be timed and charged at a higher rate.

Disclaimer

The information contained in this publication is intended only as a guide to payments and services. It's your responsibility to decide if you wish to apply for a payment and to make an application with regard to your particular circumstances.